Mheshimiwa Spika, katika Kaunti yetu ya Kilifi ni aibu sana kusikia kwamba ndio tunaongoza katika mambo ya kudhalilisha jinsia katika Jamhuri yetu ya Kenya. Ni huzuni kubwa sana lakini hata hivyo kama kuna sheria bila sera haiwezekani lakini sera hii itawezesha haya mambo kuisha na yataisha kwa sababu tulipokuwa pale Rabai jambo ambalo lilingishangaza kuna mzee ambaye alijitokeza mlemavu alioa mkewe akazaa mtoto msichana na yule mtoto msichana anaishi naye yeye. Yule mama akaondoka akaenda kuolewa na bwana mwengine na yeye anaishi na mtoto na msichana mkubwa sana na mzee mwenyewe ni mlemavu. Inahuzunisha sana ikiwa wananchi yale wanayapitia hawawezi kusonga mbele.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hata ukiangalia upande wa elimu huo udhalilishaji ambao upo ni mkubwa sana. Karibu kuna wengi ambao hawawezi kupata msaada bila kudhalilishwa na yuko tayari adhalilishwe kwa sababu hana jambo la kufanya na hana mahali pa kuenda. Ni aibu kubwa sana na tunastahili kuwa na sera hii na wale maafisaa ambao watakuwa karibu kila wadi wataweza kutusaidia kujua nini kinaendelea kwa sababu hata wengine utakuta wako na familia zao; baba na mtoto wanafanya mambo ambayo si ya haki lakini hawezi kuenda popote kwa sababu ya uoga ukiyapeleka mbele yule atakayekusaidia ni nani. Tukiwa na hizi nyumba ambazo akiwa mtu amepata haya madhara anaweza akachukuliwa na akahifadhiwe na aweze kupata mahitaji yake basi kutakuwa na uwazi ya kwamba mtu anaweza akajitokeza na kutoa yale ambayo anayapitia.

Kwa hivyo, naomba Bunge hili kuweza kupitisha hii sera ili kuweza kubadilisha hii hali ya udhalilishaji katika Kaunti yetu ya Kilifi. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana na naamini kabisa sote tutaona umuhimu wa sera hii maanake hii sera italinda kizazi ambacho tuko nacho sasa hivi na pia kizazi ambacho kinakuja. Asante, mheshimiwa Spika, na naunga mkono.

*(Question proposed)*

**Hon. (Ms.) Mariam:** Asante, Bw. Spika, kwa fursa hii. Nasimama kuunga mkono hii Ripoti ambayo imeletwa na mheshimiwa Agnes Sidi ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maswala ya Jinsia. Dhulma za kijinsia ni jambo ambalo limeendelea kwa mda mrefu sana na sisi kama Kilifi ikifika magatuzi tumekuwa tukiorodheshwa namba moja katika hayo maswala kumanisha hayo maswala sisi tunayatekeleza zaidi kushinda mahali kwengine.

Dhuluma za kijinsia ni ukiukaji wa haki za kibinadamu na, Bw. Spika, Katiba yetu ya Kenya ilipata sifa sana kwa sababu ukiangalia sura ya nne, ambayo ni sura ndefu zaidi ndani ya ile Katiba, inazungumzia kuhusu maswala ya haki za kibinadamu na sisi kama Kilifi tukiwa ndani ya Kenya, kumanisha tuko na Katiba ambayo iliweka mikakati ya kuhakikisha kuwa hizi dhuluma hazitakuwa kabisa. Na ikiwa sura hii ndio ilitupatia sifa na Katiba yetu kuonekana kuwa ni Katiba ya maana kitu ambacho kilibaki ni hii sera na mimi nikisimama hapa naweza sema leo ni siku ya historia kwa sababu mchakato mzima wa hii sera ilianza mwaka wa 2016 kama sikosei kabla hata sijafika katika Bunge hii.

Nimechangia hii sera nikiwa ule upande mwengine ambao tulikuwa tunasema sisi ni watetezi wa haki za binadamu. Tumeshirikisha serikali ya gatuzi hili mara nyingi na kuna mashirika mengi ambayo hata lile ambalo nilikuwa mimi najihusisha nalo tumetumia fedha kuhakikisha kuwa hii sera imepita na pengine kwa hali fulani kuanzia huo mwaka haikuweza kuona mwanga ama kufika katika hii Bunge. Kwa hivyo, nikisema ni siku ya kihistoria namaanisha leo hata wale ambao tumechangia hii sera tukiwa kule upande mwengine kwetu hii siku ni siku muhimu sana pamoja na sisi kama Bunge kwa sababu tukipitisha hii sera, hii sera ndio itatupa muongozo wa kuhakikisha kuwa hizi dhulma hazitatekelezwa ndani ya hili jimbo letu. Naunga mkono mia fil mia hii Ripoti. Asante, Bw. Spika.

**Hon. Mohamed:** Asante, Bw. Spika. Mimi pia niungane na wenzangu kuunga mkono sera hii ambayo imeletwa na Kamati ya Jinsia. Ni kwamba kweli kumekuwa na dhuluma za kijinsia ambazo tunaona ya kwamba kaunti yetu kwa bahati mbaya ama kwa masikitiko kwamba inaweza kuwekwa mbele katika hali hizi na Katiba yetu kama mtangulizi mheshimiwa aliye kuwa kwa sakafu ametuambia tu kwamba kila mmoja ana haki. Hapa kwetu Kilifi ukifika uzee haki yako imeisha maanake ukianza kutoa mvi wewe ni mchawi.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hapa Kilifi, umasikini unatuweka katika hali ambayo tunapata dhuluma sana. Unapata ndungu zetu, dada na hata sisi maanake pia, Bw. Spika, tuanze kujitetea kama watoto wa kiume maanake sasa naona tumeachwa sana wengi wamekimbilia kwa mtoto wa kike na mtoto wa kike kusema ule ukweli kwa sasa amepata kuangaziwa na kwamba kwa njia moja ama nyingine ameanza kuwa mahali salama. Lakini mtoto wa kiume ameachwa wazi sana ndio maana utapata wengi tuko kule majumbani tunapigwa na bibi zetu lakini hatuwezi kujitokeza kwa urahisi na kusema kwa sababu unapata ile aibu ya kusema mimi ndio... bwana itakuaje nianze kuambia polisi ati bibi yangu usiku amenipiga.

Kiukweli ni kwamba ni dhuluma; haifai kuendelea hawa ndugu zetu ama binti zetu waelewe kwamba hata sisi tuna haki. Ikiwa wao wana haki hata sisi tuna haki. Kwa hivyo, sisi pia haki yetu ilindwe lakini pia tuseme tu isiishie hapa kwamba sera tumeipitisha na utekelezaji wake usiweze kutekelezwa.

Mimi hupenda kupeana mifano kwa sababu ni mkaaaji na ni mtu ambaye nimekaa karibu sana na wananchi wangu kule Bamba. Inasikitisha kuona ya kwamba visa vingi haswa vya dhuluma za watoto wa shule ambao wanapata uja uzito wa mapema zinashindwa kufika katika mahakama kwa sababu ya asasi za kiusalama ambazo tuko nazo kule nje. Utapata mzazi ameweza gundua ya kwamba mtoto wake ambaye bado yuko shule na anafaa kulindwa na jamii pamoja na serikali ameweza kupata ujauzito. Atachukua swala hilo na kulipeleka hadi polisi. Lakini utashangaa baadaye polisi yule yule aliyepelekewa ndio ataanza kupeana mawaidha kwa mzazi yule wa pili kuweza kutoa ile kesi mahali inastahili kufika ili haki isipatikane.

Ningeomba ya kwamba tupitische kama Bunge kisha tuhakikishe kwamba utekelezaji wa sera hii umeweza kufanywa asilimia mia moja. Hiyo ndio itaweza kutusaidia ili tuone ya kwamba visa hivi vinarudi chini. Nikiunga mkono pia najua, Bw. Spika, wakati ule ulipokuwa Mbunge wetu wa Ganze uliweza kusaidia sana wale wazee wenye mvi kuweza kuwapatia mahali wakawa wanaishi kwa sababu kule kwao ama kule majumbani tulikuwa tunawaita wachawi lakini tukawa tunasema si haki ya kwamba kila mwenye nywele nyeupe basi tayari ni mchawi.

Ni mambo ambayo yanasikitisha na utapata sababu hizi nyingi si uchawi ila ni kwamba baadhi ya ndugu zetu ambao hawana kazi ya kufanya hutetea urithi tu. Sasa urithi unapelekea kuita babako mchawi kwa sababu unamtafutia sababu ya kumwondoa duniani uweze kupata kile alichonacho. Kiukweli ni kwamba tabia hii inafaa kukemewa na sera hii iweze kutupatia mwongozo ili visa hivi viweze kupungua Kilifi na wazee wetu kwa sababu hao ndio urithi wetu mkubwa hata kiupande wa ushauri.

Sasa utapata, maboma mengi hayana ushauri na mambo yanaenda sivyo kwa sababu wazee wengi hawapo. Kwa hivyo nafikiri sera hii itatusaidia, hivyo basi niombe Bunge hili tukufu, tuweze kuunga mkono sera hii na tuweze kuipitisha na kisha kuna ile Kamati ambayo huwa inasimamia utekelezaji wa mambo kama haya. Tufuatilie na kuhakikisha kwamba utekelezaji wake umeweza kufanywa asilimia mia moja. Asante, Bw. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hoja hii. Ninaunga mkono kupitishwa kwa sera hii.

**Hon. Brown:** Asante sana, Bw. Spika, kwa nafasi hii ambayo maulana ametujalia tuwe hapa kwa ajili ya kazi wananchi walivyotupatia. Mimi wacha niwe mmoja wa kuunga mkono Hoja hii na nikijua kwamba hapa hili ni Bunge, na Bunge ni mahali pa mjadala kila mbunge ambaye ameletwa hapa ni fursa yako wewe uwe na nafasi ya kuwa na maelezo ya kueleza wananchi; kueleza umma wote ili watu wapate ufasaha na elimu katika mijadala yote ambayo tunaipitisha hapa. Sio vyema tupitische mijadala ambayo hatujaijadili wala hatujaifafanua si vyema katika Bunge hili.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mimi ningelipenda kupeana changamoto maana sikueleweka pale mwanzo nilikuwa ninanyosha mkono nikaonekana ni kama ninapinga; nilikuwa sipingi lakini nilikuwa na Hoja, lakini pia naamini na ninashukuru kwa sababu tumeipitisha na ninaamini itaenda kufanya vyema. Katika mjadala wa leo wa kijinsia ni mjadala ambao ni wa maana sana. Na kusema ukweli ninaunga mkono wale wanenao waliokuwa hapa wakizungumzia haswa ningepeana kongole, mheshimiwa Spika, kwa hatua ulizozifanya katika utatuzi wa wazee wetu ambao walikuwa wakiishi *especially* sehemu zile za kule Ganze.

Kusema kweli, kule kwetu sehemu za kule Chonyi na sehemu nyingine nyingine kuna baadhi bado wanatekeleza vitu kama hivi na visanga kama hivi. Lakini jambo la maana ni kwamba hii tukiipitisha la umuhimu ni serikali yetu ya Kaunti ipate uwezo wa kuhakikisha kwamba mambo haya yanatekelezwa. Mimi kabla kuja Bunge nimekuwa sana katika ulingo wa kusimamia watu wasio na uwezo kwa viungo vyao. Na katika maisha yangu yote nilipotoka shuleni hiyo ndio imekuwa kazi yangu kuhakikisha kwamba napeana utetezi na kuhakikisha kwamba Hoja kama hii ingefika ili kupata uteteti.

Kuna umasikini ndani ya watu ambao tuseme kwamba ni walemavu lakini kwa lugha sanifu haistahili tuwaite namna hiyo. Ni watu ambao hawana uwezo katika sehemu ya viungo. Mheshimiwa Spika, unaweza kufikiria mtu amezaa watoto wake kama watano mtu huyu hana uwezo wa kutembea na hapa anatakikana watoto hawa wapate elimu, wapate chakula, wapate mavazi na wapate kila kitu chao. Hapa ndio huwa mara nyingi hii hali inawakumba hawa ndugu zetu na mama zetu. Nikiamini serikali yetu ikiwa itaangazia jambo hili hakika itaangamiza umasikini ndani ya Kilifi hii.

Mambo haya yameongezeka kwa sababu jamii hii haina mtu anaingalia. Hata saa hii nikiuliza pengine *statistics* ya wale ambao wako katika hali ya ulemavu hakuna mtu anajua *statistics* na familia zao ama tegemeo lao ni nini. Hii itakuwa ni jicho kubwa la kusaidia sana familia kama hizi zipate kuangaliwa. Utaona baba mzima, mtu ni mlemavu, yeye hawezi ongea, yeye hawezi sikia, wala hata kuinuka mtu anaenda kufanya unajisi ati kisingizio wanasema ati ni uganga fulani anaenda kujiosha. Huu ni uchawi na mambo kama haya yatakuwa yanatusaidia sana kufanya nini? Kuweza kukamata watu kama hawa. Ni jambo la kuhuzunisha hakuna mtu aliyeomba kuwa mlemavu; ni jukumu letu sisi kama viongozi tuliochaguliwa tuhakikisha kuwa tuko na uwezo wa kutetea watu kama hawa. Nataka kuzungumzia maswala ya Elimu nataka kukanusha katika mjadala ule tuliozungumzia hapa kwamba wale hawakupata uwezo wa kuenda mbele wasomee mbele...sasa kusomea mbele kiviipi na masomo ni masomo ujuzi ni ujuzi mtu alichangua kuwa fundi wa kutengeneza saa, yule amechagua kuwa fundi wa chuo kikuu, elimu ni kitu kinatukumba hapa...

**The Speaker** (Hon. Mwambire): There is an intervention from hon. Morris, please take your seat.

**Hon. Hinzano:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa aliye kwa sakafu anaturudisha nyuma na sisi tuko katika sera ya jinsia na Utamaduni ili kuhakikisha kwamba tunaongea mambo yanayodhalilisha wananchi, asimame tu kwa mjadala ili atusaidie ili tupate ufahamu mzuri asichanganye wananchi.

**The Speaker** (Hon. Mwambire): Hold on there is another intervention from Hon. Ziro.

**Hon. Ziro:** Asante sane, Mheshimiwa Spika. Mnenaji ametupa msamiati ningetaka afafanue kwa sababu sikusikia kwa mheshimiwa yoyote kwa “ukikosa kwenda mbele somea mbele” sijui anamaanisha nini.

**The Speaker** (Hon. Mwambire): Stick to the Motion on the Floor.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

**Hon. Brown:** Asante sana. Sijui wenzangu akili zao ziko wapi, katika mtiririko ninaozungumzia ni kwamba kule kukanusha ya kwamba mtu akienda chuo cha ufundi ni kama hajaenda shule, yaani anaona akienda chuo kiku ndio ameenda shule, wengi wanaenda chuo cha ufundi kwa sababu anataka kuwa fundi...

**The Speaker (Hon. Mwambire):** Huwa wanadhulumiwa vipi kijinsia katika muktadha kama huo?

**Hon. Brown:** Katika kuinua hali ya kijinsia ni kwamba ni serikali yetu iwe itajizatiti katika kuangazia jinsi ya vile tutainua walio chini katika umaskini maana umaskini ndio unakidhiri ndio unatufanya sisi mara nyingi watu wetu wanakosa nafasi za kujinasua katika mizozo hii. Lazima kubuniwe taasisi za mafunzo ya kuhakikisha kwamba wale waathirika... ambao mimi nina kama wawili ninawapa madawa maana wamedhulumiwa ki mapenzi jambo kama hilo ni la kuongezea katika mjadala huu. Ninaunga mkono lakini kuwe na vikao vya kuwezesha Kaunti yetu iboreshe mjadala tulio nao. Naunga mkono Hoja hii.

**Hon. Mkadi:** Asante sana, Mheshimiwa Spika, kwa hii nafasi. Yapo mengi yameongelewa kuhusu huu mjadala. Naomba nisisitize kwamba kipindi kilichopita niliajaliwa kuwa katika kamati hii na swala hili la udhulumiwaji wa kijinsia tuliliongea kwa mapana kuna mengi yalipitishwa lakini upande wa utendaji kazi hawa wenzetu hawatilii mkazo. Nina furahi kwamba katika zile Kamati ambazo Mwenyekiti amezitaja kwamba kutakuwa na kamati upande wa County Level na Ward level labda hiyo inaweza kusaidia. Kutoka kule chini vijijini mpaka kufikia kule haki ingepatikana labda kulikuwa na hatua ndefu. Kwa sasa, kuna kamati mbili ambazo zimeundwa ili kusaidia katika kutekeleza sera itakuwa hatua nzuri. Kwa hiyo, naunga mkono.

**Hon. Paul:** Asante kwa nafasi hii. Kwanza nataka nipongeze Kamati kwa kuchukua maoni mbali mbali na kuleta sera hii hapa Bungeni. Nasema kwamba kulingana na hali ilivyo kule mashinani hasa kule kwangu Magarini, kuna sehemu nyingi ambazo wasichana na pia wavulana wamedhulumika kwa sababu kulikuwa na ukosefu wa sera kama hii. Wamedhalilishwa wakionekana mtu ana dhulumika na hapati haki yake.

Leo yale ambayo Kamati hii waliketi wakiongozwa na mheshimiwa Sidi wa Kayafungo ninaunga mkono mia kwa mia ya kwamba sehemu zile zilizo mstari wa mbele kama za uchimbaji mchanga, mawe, madanguro na sehemu za kulewa wasichana wamedhulumiwa. Kupitia kwa sera hii nina hakika kwamba tukiipitisha hapa ninaamini kuwa hakuna mtu yeyote atadhulumiwa na kama mtu akidhulumiwa na njia hii iliyowekwa hapa ifwatwe vilivyo basi watapata funzo. Mwaka jana, mzazi mmoja alilala na msichana wake mpaka mtoto akapata ujauzito na mambo yanaenda tu bila mtoto kupata haki yake. Lakini kupitia kwa seri hii hatua zitachukuliwa ili wanaopatikana katika mambo kama haya wachukuliwe hatua kwa haraka. Utendaji kazi utaanza chini katika *Ward level*. Nasimama kuunga mkono.

**Hon. (Ms.) Faith:** Asante sana, Mheshimiwa Spika. Napenda kuwakaribisha wageni wetu waliokuja kwa sababu ya *agenda* hii. Nataka kushukuru sana Kamati ya *Gender, Culture* na *Social Services* kwa ile kazi kubwa ambayo wamefanya kupitia wananchi Kilifi yote ili kuchukua mawazo yao na maoni hivyo nataka kuwashukuru sana kwa kazi hiyo. Kitu kingine ambacho kimenipa motisha zaidi katika hii Kamati ni mawazo yaliyotolewa na wananchi yakiwa yatatekelezwa. Kwanza nataka kusema naunga mkono mia kwa mia mswaada huu ulioletwa hapa Bungeni.

Nataka niseme hivi. Umegusia mambo mengi ambayo yakifwatiliwa, hizi dhuluma za kijinsia kwa mrengo wowote wa binadamu kuanzia juu mpaka chini ninamaanisha wanaume,

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

wanawake, watoto walemavu na wote watakuwa wamesaidika. Kitu cha kwanza ambacho kinanipa kujua kwamba tutasaidika ikiwa hii sera. Kwanza, Bw. Spika, tumesema tukipata zile *safe houses* za hawa waathiriwa. Vile ambavyo wamepanga wananchi wametaka hizi nyumba za usalama za waathiriwa ziwekwe mahali ambapo ziko karibu nao ili waweze kufichwa. Litakuwa ni jambo zuri sana.

Swala lengine ambalo wananchi wanaomba; walitaka kuwe na laini ya simu ya moja kwa moja (*Free toll service*) yaani wakipatwa na dharura kama hiyo ama wakidhulumiwa kijinsia wawe wanaweza kupiga simu ya moja kwa moja ili kuripoti kesi kama hiyo. Swala lengine, Mheshimiwa Spika, kuna kule watu wanadhulumiwa. Kwengine umefanya umedhulumu mtu ama ukasingiziwa lakini wewe mtetezi wako ni nani? Hii sera imesema kuwa itahakikisha inawalinda mashahidi walio nao na wanadhulumiwa na kupiga ripoti. Kuna watu wengine wanaweza kufuata wale mashahidi wakawaangamiza ili wapoteze ushahidi. Lakini tukiwa tuna nyumba za kuwaficha hawa mashahidi, haki kwa yule mtuhumiwa itapatikana. Haya yote ni maoni yaliyotolewa na wananchi wa Kilifi.

Jambo lengine na ningependa niseme Kiingereza, *systems for tracking GBV cases and interventions*. Yaani tuwe na mpangilio kabambe wa kuhakikisha ikiwa msichana amedhulumiwa pengine na *state officer* ama mlinda usalama tunafuatilia vipi mpaka tuhakikishe haki ya yule mdhulumiwa imepatikana? Sasa hapo tunahitaji kufuatilia kwa msururu bila kupoteza ushahidi. Hili pia ni wazo wananchi walilileta kwa lengo la kuwa hakuna mtu ambaye ana haki ya kudhulumiwa; awe maskini au tajiri kila mtu ana haki ya kupewa uhuru wake wa kuishi kama mtu mwengine.

Swala lengine waliomba Kaunti itenge pesa za kutosha kwa sababu huku kufuatilia haya mambo ya kudhulumiwa kwa kijinsia inafatefate nyingi. Mimi kule ninakotoka ikiwa natokea Ganze, kuna kijana wa shule alisemekana amebaka mtoto lakini wengine wakawa wanasema amebakwa na ndugu yake. Kwa kuwa huyu aliyebakwa hana mtetezi, ile kesi imemlalia. Mheshimiwa Spika, watu kama hawa wanaodhulumiwa kwa kuwa hawana utetezi, ni nani ambaye ni wa karibu wa kuwatetea watu kama hawa? Ndio maana tunahitaji sera kama hii ikija iwe itatetea mtu kama yule.

Lengine na la mwisho ningependa niwe wa mwisho. Ningependa kusoma kwa Kiingereza, *Government related activities between the National and the County Government*. Hivi ni vita ambavyo hatuvitetei sisi peke yetu. Mheshimiwa Spika, wewe ukikumbuka wazee wetu wanauwawa. Hawauwawa kwa Kaunti peke yake; kisa wanasemekana ni wachawi. Hata huko juu pia wanauwawa lakini tukiwa tutashirikiana na serikali kuu maana hao tunawahitaji wakati kumefanyika jambo kama lile.

Yaani ukiwa na mvi kama vile mimi, wewe kweli ni mchawi? Mheshimiwa Spika, kama si dhuluma za kijinsia hizi ni nini? Sasa mimi kesho nikisongasonga nitaambiwa mimi ni mchawi ama sijui itakuaje maanake wananchi wamekuwa hawataki kuona mtu mwenye mvi. Hii ina ashiria nini? Tutamaliza wazee wetu Kilifi kwa sababu wana mvi lakini sasa tunataka uhusiano mwema baina ya Serikali kuu na Serikali ya Gatuzi ili tuhakikishe hii sheria imefanya kazi vizuri. Kuna vitu ambavyo tunavhitaji kuitia nguvu. Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa kunivumilia.

**The Speaker** (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Faith anasema yuko na mvi kwa hivyo anaweza hofiwa hata Spika amepevuka kidogo na nimemuona mdogo wangu hon. Mohamed pia anaweza kuwa mshukiwa kule mtaani. Leo ni Jumatano ni siku ya kuongea lugha ya Kiswahili.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Wale ambao wamezoea kuongea Lugha ya Kiingereza naona wanatatizika lakini mtazoea tu msiwe na hofu. Mheshimiwa Jambo wa Jilore.

**Hon. Jambo:** Asante, Bw. Spika, kwa nafasi hii. Mimi pia naunga mkono haya maswala ya kijinsia. Mengi yamezungumzwa. Wananchi wa Kilifi wako machoni katika Bunge hili Tukufu kuona ya kwamba hii Hoja imepita. Waswahili husema moto ukizimika jivu litakosa thamani. Sioni sababu nyengine iliyobaki ikiwa leo itapita, jana itaitwa juzi. Msafara huu ulianza kutokea huko zamani wacha leo tutie kikomo kwa kupisha hii. Asante.

**The Speaker** (Hon. Mwambire): Hon. Morgan Kubo.

**Hon. Kubo:** Asante sana, Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii. Nishukuru Kamati kwanza kwa kuleta hii Hoja hapa Bungeni. Nimesimama kuunga mkono haswa nikisikitikia Wadi jirani ya Mwawesa wazee wanauwawa; kila Jumamosi tunazika. Hilo jambo limenihuzunisha sana kwa sababu iko Rabai. Kila jumamosi Mwawesa tunazika mzee ambaye ameuwawa kwa hutuma za uchawi.

Ninaamini ya kwamba hii Hoja itasaidia pia kumaliza maafa ya Mwawesa. Kwetu Kambe-Ribe tuliyamaliza miaka ya kuhesabu hakuja uwawa mzee. Kabla sijaingia Bungeni niling'ang'ana na hilo jambo hata nikanyimwa kura sababu ya jambo hilo. Ikaisha na nina shukuru niliingia hapa Bungeni lakini kwa hii Hoja ya leo tunaangalia sana Mwawesa tuone kama itamalizika. Asante sana, Bw. Spika.

**The Speaker** (Hon. Mwambire): Hon. Ziro.

**Hon. Ziro:** Asante sana, Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii japo ni kuchelewa kwa sababu mengi yamezungumziwa. Ningetaka nipongeze Kamati kwa kuleta hii Sera hapa Bungeni na nitasema imechelewa kwa sababu watu wengi wameteseka; wengine wameuwawa na kudhulumiwa kijinsia. Ningetaka kusema ya kwamba tunapoongelea kuhusu dhuluma za kijinsia tuisahau vijana. Maanake naona katika wadi nyingi ambazo nimeweza kutembela hapa Kaunti ya Kilifi hasa kule shuleni, naona mashirika yameangazia sana masomo ya wasichana na yule mvulana sasa ni kama anaanza kupotea. Ukiangalia mitandao, kila wakati utaambiwa msichana ambaye amefanya vizuri na hana uwezo. Imefikia wakati tuweze kuangalia mtoto wa kiume kwa sababu kama hatutakuwa makini pia naye huenda ikafikia mahali akawa haonekani mahali popote.

Pili, ningetaka niunge mkono Sera hii kwa kutuletea Kamati kwa kila wadi. Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba kama vile mheshimiwa wa Bamba alivyosema, wale wanaume pia wako na yao ya kusema lakini imekuwa ngumu sana kuenda polisi kushtaki kwamba pia hao wanadhulumiwa na wake zao kwa majumba. Tukisema kudhulumiwa haki zao, kuna zile shughuli za nyumbani.

*(Laughter)*

Mheshimiwa Spika, kuna wengine wanaumia lakini wamekosa mahali pa kulilia. Tunapopata hizi kamati kwa Wadi, inaaminisha kuwa kutakuwa na urahisi hawa wazee pia waweze kuwa na uhuru wa kuweza kueleza matatizo yao na hatua iweze kuchukuliwa. Asante sana Mheshimiwa Spika.

**The Speaker** (Hon. Mwambire): Allow me to call the Mover to respond, Hon. Sidi.

**Hon. (Ms.) Sidi:** Thank you, Mr. Speaker. Once again, I would like to thank the public, our stakeholders, the Department, the Committee Members and the Clerks for this good job that was done. I would want to inform the public that this one does not stop here; we will work

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

together with the Department to ensure that budget allocation has been given to these policies and we have safe houses and committees in place.

We use dispensaries right now as our safe centres. For the youth, we can encourage them to apply for Wezesha Fund to elevate the poverty levels. Civil education will continue, Mr. Speaker, and we will work with the Implementation Committee to ensure this Policy is followed to the letter so that we are not leading again from the front as Kilifi County in GBV, but we lead from behind. Thank you, Mr. Speaker, and everyone who participated. Thank you.

*(Question put and agreed to)*

**The Speaker** (Hon.Mwambire): I think now the Committee on Implementation will follow it up as required.

## ADJOURNMENT

### SHORT RECESS

**The Speaker** (Hon.Mwambire): Hon. Members, we have come to the end of those deliberations. We are adjourning today pursuant to Standing Order 25(3) for the Third Session-First Part for short recess which is starting on Thursday, 28<sup>th</sup> March 2024 to Friday, 12<sup>th</sup> April 2024. The House will resume its sittings on Monday, 15<sup>th</sup> April 2024. The House stands adjourned, but you may be called for a Special Sitting in case any matter arises.

The House rose at 4:05 p.m.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*